Sensa ya 2020 ni nini?

02 Ni kwa nini ni muhimu sana?

- Kwa namna ile ile tunavyopiga bajeti ya fedha zetu kwa mahitaji na idadi ya watu kwenye familia yetu, serikali inahitaji taarifa kutoka kwa Sensa ili kutambua namna ya kutenga fedha kwa programu kadhaa katika Jamii, kama vile:

Programu za Utunzaji wa Kiafya
Medicaid, WIC, Utunzaji wa Watoto, n.k.

Miundombinu ya Umma
Ujenzi na utunzaji wa barabara, Usafiri wa umma

Elimu ya Umma
kujenga na kutunza shule za umma, elimu maalum na elimu kwa watu wazima

Nyumba za bei Nafuu
Kuzisaidia programu zinazotoa nyumba kwa watu wa kipato cha chini

- Kadri idadi ya Sensa inavyokuwa sahihi zaidi kwenye Jamii zetu, ndivyo fedha zaidi hutengwa kwa jamii zetu kwa miaka 10 ijayo!

Usalama wa Taarifa za Kibinafsi 04

- Kisheria, data za Sensa zinaweza kutumika kwa madhumuni ya kitakwimu tu. Taarifa za kibinafsi zilizokusanywa na Ofisi ya Sensa hazitolewi kwa idara nyingine yoyote ya serikali.
- Taarifa za kibinafsi za sensa haziwezi kufichuliwa kwa miaka 72 (ikiwemo majina, anuani, na nambari za simu).
- Watu wanaofanya kazi ya sensa huapa kulinda taarifa hii; endapo wakaivunja sheria hii ya shirikisho wanaweza kutiwa jela au kutozwa faini kubwa!

Ni lini NitaikamilishaFomu Yangu ya Sensa ya 2020? 06

- **Katikati ya Machi 2020 -** Watu wanaweza kuanza kujibu maswali ya sensa kwenye mtandao wa intaneti na simu; fomu za makatarasi zitatolewa kwa familia zilizopo kwenye maeneo yenye ufikiwaji hafifu wa intaneti au kwa kuombwa.
- **Mei 2020 - Agosti 2020 -** Ufuatiliaji kwa wale ambao hawajapeana majibu yao: Yeyote ambaye hatakuwa amejibu au kujaza fomu za sensa kufikia mwisho wa Aprili 2020 atalazimika kutembelewa na mfanyakazi wa Ofisi ya Sensa nyumbani kwake kufuatilia na kumsaidia kujaza fomu hiyo ya sensa.

01 Sensa ya 2020 ni nini?

- Katiba ya Marekani inaitaka serikali ya shirikisho kumhesabu kila anayeishi humu nchini kwa kila miaka 10.
- Sensa lazima ihusishe watu wa umri, rangi na kabila zote; raia na wasio-raia wote, bila ya kujali hadhi yao ya uhamiaji. Ushiriki wetu ni haki na ni wajibu.

Ni Nani Anahesabiwa? 03

- Kila mmoja kwenye familia anatakiwa kuhesabiwa!
- Wanafamilia wote ikiwa ni pamoja na watoto wachanga, watoto, wanafunzi wa vyuo, watu wazima, ndugu, marafiki, watoto wa marafiki, bibi na babu, wakwe, n.k., bila ya kujali umri wao au hadhi yao ya kisheria.

Unaweza Kujaza Kivipi? 05

- Sensa itapatikana mtandaoni, kwa simu, na karatasi.

- Fomu ya Sensa ya mtandaoni itapatikana kwa lugha 13 tofauti. Pia Sensa itapatikana kwa njia ya simu katika lugha 59. Kutakuwa na mwongozo mtandaoni wa namna ya kuijaza sensa kwa lugha 59.
- Unapojaza sensa hakikisha kuwa kila mtu anayeishi kwenye familia anahesabiwa.

Nini Kitatokea Endapo Hutajaza Fomu Hiyo? 07

- Mfanyakazi wa sensa atakuja nyumbani mwako kukusaidia kujaza fomu endapo utakuwa hujajaza sensa kufikia mwisho wa Aprili 2020.

Je Wajua.....

- Idadi ya viongozi wanaochaguliwa kwa serikali za mtaa, jimbo, na shirikisho inategemea Sensa?
- Tennessee inaweza kupata kiti kimoja zaidi kwenye Baraza la Wawakilishi wa Marekani kwa matokeo ya Sensa ya 2020.
- Wilaya pia hupangwa upya kwa kutumia takwimu za Sensa. Hii inajumuisha: Wawakilishi wa Shule za Wilaya | Halmashauri ya Jiji | Jimbo | Baraza la Wawakilishi la Marekani

Kwa taarifa zaidi piga simu kwa 615-414-1030 au umtumie barua pepe Cesar Bautista kwa cesar@tnimmigrant.org

Tennessee Immigrant & Refugee Rights Coalition · La Paz Chattanooga · Latino Memphis · centro Hispano de East TN